BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Sita – Tarehe 12 Mei, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2026/2027.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka 2026/2027.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC):

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) kwa Mwaka 2026/2027.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

358. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Muungano wa nchi mbili huru, Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Je, Serikali inatambua kwamba zipo kasoro na changamoto ambazo zinahatarisha Muungano wa nchi mbili hizi.

### Wizara ya Fedha na Mipango:

125. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Hivi karibuni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alinukuliwa na vyombo vya habari akisema kuwa, kutegemea mapato kwa kuweka faini ni mambo ya kikoloni na unyang'anyi. Kauli hiyo inaakisi baadhi ya taasisi zetu hapa ndani, kuweka viwango vya faini vikubwa ambavyo haviendani na uhalisia wa vipato vya wananchi, kama vile kuweka faini kwa kiwango cha shilingi laki tatu (300,000) ambazo ni sawa na kima cha chini cha mshahara wa mtu.

(a) Je, Serikali imeweka sera au muongozo upi maalumu wa namna ya kuweka viwango vya faini ili visionekane kuwakomoa wananchi.

(b) Kwa nini utaratibu wa taasisi zetu wa kutegemea faini kama vyanzo vya mapato usionekane kuwa umepitwa na wakati na kama alivyosema Waziri Mkuu kuwa ni wa kikoloni na unyanga'anyi.

(c) Je, ni lini taasisi zetu zitakaa na kubuni vyanzo vyengine vya mapato badala ya kutegemea mapato kwa kuweka viwango vikubwa vya faini.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

5. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

   Wananchi wanaoitumia barabara kutoka Chimba kuelekea Mambosasa na kutokezea Konde Mahakamani Pemba, wameendelea kupata shida kubwa na usumbufu usiomithilika kutokana na ubovu wa barabara hiyo. Wengi wao hawawezi kuitumia barabara hiyo isipokuwa waendesha vyombo vya moto vya maringi mawili na baskeli, wakati barabara hii ni ya asili na imezoeleka sana.

   Ni zipi sababu zinazokwamisha kujengwa kwa kiwango cha lami barabara hiyo.

266. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

   Serikali iliwaeleza wananchi kwamba Meli ya MV. Mapinduzi II imeshakamilika kufanyiwa matengenezo na ipo tayari kuanza kazi zake lakini kikwazo ni kutokukamilika kwa Bandari ya Mpiga Duri.

   (a) Je, ni lini bandari hiyo itamaliza na kuanza kutumika.

   (b) Kwa nini Serikali haioni kuwa inapoteza mapato mengi kutokana na kuiacha Meli ya Mapinduzi II nangani.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

413. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

   Serikali ina mpango gani wa kuimarisha vikundi vya wanawake katika Mkoa wa Kusini Pemba ili wapate fursa za masoko, mafunzo na mitaji.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

314. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumekuwepo na ongezeko la bei za vifaa vya ujenzi hali inayochangia kuongezeka gharama za ujenzi na kuathiri uwezo wa wananchi wengi kumudu kumiliki nyumba zao binafsi.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kisera na kiutendaji ya kudhibiti mfumko wa bei za vifaa vya ujenzi.

## <u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasilisili na Mifugo:</u>

304. MHESHIMIWA JUMA USONGE HAMAD (Jimbo la Chaani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada za kuwasaidia wakulima hususani kwenye ujenzi wa mindombinu ya Kilimo cha Umwangiliaji hapa Zanzibar.

(a) Je, ni kwa kiwango gani kwa sasa wakulima wa Bonde la Kinyasini wamenufaika na uzalishaji wa mpunga katika bonde hilo.

(b) Je, ni wakulima wangapi waliopatiwa *plot*s za kilimo cha mpunga katika Bonge la Kinyasini.

## <u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

253. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na uwepo wa matokeo mabaya ya mitihani katika visiwa vidogo vidogo hapa Zanzibar, kama vile kisiwa cha Makoongwe, Kisiwa Panza na Kojani.

(a) Ni sababu zipi zimepelekea matokeo kuwa mabaya katika skuli hizo.

(b) Serikali imeandaa mikakati gani ya kukabiliana na changamoto hii ya matokeo mabaya katika visiwa hivyo.

477. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika skuli saba zilizomo ndani ya jimbo la Wingwi, upo upungufu mkubwa wa walimu wa masomo mbalimbali.

(a) Je, Serikali inalifahamu vipi tatizo hili.

(b) Je, ni lini changamoto hii itapatiwa ufumbuzi.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

484. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Pamoja na Serikali kukusudia kupanua na kuongeza nguvu kwenye michezo kwa kujenga viwanja vya mpira vya kisasa, hadi sasa ndani ya kisiwa cha Pemba ni Uwanja wa Gombani pekee ndio uliojengwa.

(a) Ni lini Serikali itavijenga viwanja vya mpira vya Pemba kama ilivyovijenga vya Unguja.

(b) Ni lini viwanja vya mpira katika jimbo la Wete vitajengwa, huku ikifahamika kuwa ndio sehemu ambayo mpira wa miguu unapendwa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

10. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitengeneza au kununua meli mbili kwa ajili ya uvuvi katika Bahari Kuu.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika kutengeneza au kununua meli hizi.

(b) Je, hadi sasa ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kupitia shughuli za meli hizi.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

319. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utawala Boara:

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi kuhusu ucheleweshaji wa baadhi ya huduma za umma hata kwa zile huduma zinazopaswa kutolewa kwa muda mfupi. Hali hii husababisha usumbufu kwa wananchi na wakati mwengine kufungua mianya ya vitendo vya rushwa.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za umma.

(b) Je, ni mikakati gani imewekwa kuhakikisha huduma za umma zinatolewa kwa wakati unaostahili katika taasisi za Serikali.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2026/2027.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**12 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**